



**MKOA WA KIGOMA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU**  
**(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**



Simu Na. +255 028 2810339  
Fax Na. +255 028 2810339  
E-Mail/Baruapep:ded@kasuludc.go.tz  
Website:www.kasuludc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
S. L. P 97,  
Kasulu — Kigoma,  
**TANZANIA.**

Kumb Na. KSDC/S.2/19/46

17/02/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu anapenda kuwatangazia wataanzania wote kuwa Ofisi imepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi chenye Kumb.Na.FA.170/358/01/C/101 cha tarehe 27 Januari, 2022 kwa ajili ya kutangaza nafasi ya Dereva daraja II kwa masharti ya kudumu hivyo wenye sifa mnaombwa kuomba nafasi ya kazi kama ifuatavyo:-

**1.0: DEREVA DALAJA LA II - NAFASI 1**

**A: SIFA ZA KUAJIRIWA:**

- i) Awe na cheti cha kidato cha IV
- ii) Awe na leseni daraja "E" au C1" ya uendeshaji magari
- iii) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari(basic driving course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi(VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali
- iv) Waombaji wenye cheti cha majaribio au ufundi daraja la II, watafikiriwa kwanza

**B: MAJUKUMU/KAZI ZA KUFANYA.**

- i) Kuendesha magari ya abiria na malori
- ii) Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote na kufanya uchunguzi wa magari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo
- iii) Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari
- iv) Kutunza na kuandika daftari la safari "Log-book" kwa safari zote
- v) Na kazi nyingine atakazopangiwa na Mwajiri wake

**C: NGAZI YA MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia viwango vya serikali ngazi ya mshahara ni TGS B kwa mwezi.

**D: MASHARTI YA JUMLA.**

- i) Waombaji wawe na umri kati ya miaka 18-45,
- ii) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye namba ya utambulisho wa uraia (NIDA)
- iii) Mwombaji anatakiwa kuambatisha nakala za vyeti vya Elimu (Kidato cha IV/VI), vyeti vya Taaluma (Certificate), Cheti cha kuzaliwa na Wasifu (CV).
- iv) Transcripts "Testimonial, Provisional Results na statement of results havitakubaliwa.
- v) Barua za maombi ziandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na zitumwe kwa njia ya Posta tu.
- vi) Mwisho wa kutuma na kupokelewa kwa maombi ni tarehe 01 Aprili, 2022 saa 9:30 alasili kupitia anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,**  
**HALMASHAURI YA WILAYA,**  
**S.L.P 97,**  
**KASULU.**

Joseph K. Rwiza  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**KASULU.**